| KISWAHILI |
|---|
| **028** |
| **11/11/2016 8.30 am- 11.30 am** |

REB
Rwanda Education Board

**MTIHANI WA TAIFA KWA SHULE ZA SEKONDARI, 2016**

**SOMO: KISWAHILI**

**MCHEPUO: ENGLISH- KISWAHILI- KINYARWANDA :(EKK)**

**MUDA: MASAA MATATU**

**MAELEZO:**

1. Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.
2. Karatasi hii ina maswali 19: Jibu maswali yote isipokuwa swali la 19 katika sehemu ya IV ambapo unaombwa kuchagua mada moja kati ya mbili.
3. Andika vizuri nambari yako ya mtihani na majina yako.
4. Andika vizuri nambari ya kila swali.
5. Mwandiko wako usomeke vizuri.
6. Tumia kalamu ya bluu.

**MALI AKILI BAHATI**

Matatu mnieleze, moja mkilibaini,
Nami kichwani nijaze, jambo bora hasa nini,
Mafundi mnieleze, niingize akilini,
Mali bahati akili, lipi bora duniani?

Kama nikipata mali, akili sina kichwani,
Hapo sina afadhali, mali mlinzi ni nani,
Hakuna ni muhali, heri kuwa maskini,
Mali akili bahati, lipi bora duniani?

Mali yataka mlinzi, kutunza vyema nyumbani,
Sivyo haipati mwezi, mara mtu maskini,
Jambo gani afadhali, nami nitiwe kundini,
Mali akili bahati, lipi bora duniani?

Ikiwa nina akili, mali sinayo nyumbani,
Jina huwa ni fakili, au huwa maskini,
Jambo gani afadhali, nami nitiwe kundini,
Mali bahati akili, lipi bora duniani?

Fikirini ufakili, jinsi ulivyo yakini,
Japo uwe na akili, watu hawakuthamini,
Hukusema jitu hili, lahangaika na nini?
Mali bahati akili, lipi bora duniani?

Bahati nikiipata, nitakuwa mtu duni,
Kila nitakapopita, leo kapita fulani,
Bali mali sikupata na akili si kichwani,
Mali bahati akili, lipi bora duniani?

Pesa nimeziokota, kama kumi milioni,
Na nyumbani sitapita, nazirudisha bomani,
Hakuna nilichopata, wangu ni umaskini,
Mali bahati akili, lipi bora duniani?

Fanyeni kuna mafungu, matatu yapo mezani,
Mnichagulie langu, niwe nalo mkononi,
Yote siyo haja yangu, moja ninalo ramani,
Mali bahati akili, lipi bora duniani?

Mtu ukikosa mali, huwambiwa maskini,
Ukiwa huna akili, utasemwa majinuni,
Bahati ikiwa mbali, hupendeki duniani,
Mali bahati akili, lipi bora duniani?

**SEHEMU YA I: UFAHAMU (Alama 30)**

**Jibu maswali yafuatayo kuhusu shairi hapa juu:**

1. Ni tatizo gani analo mshairi? **(Alama 2)**
2. Tofautisha mambo (maneno) matatu yanayolinganishwa na mshairi ukitoa maana ya kila moja. **(Alama 6)**
3. Katika aya ya pili mishororo miwili ya kwanza mshairi anaeleza nini? **(Alama 3)**
4. Mshairi alikuwa anataka kumaanisha nini aliposema:
   "Mali yataka mlinzi, kutunza vyema nyumbani
   Sivyo haipati mwezi, mara mtu maskini". **(Alama 4)**
5. Eleza kwa kifupi mishororo mitatu ya kwanza katika aya ya tano(5) **(Alama3)**
6. Eleza katika mistari mitano ujumbe wa mshairi katika shairi ulilolisoma hapo juu. **(Alama 5)**
7. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi: **(Alama 5)**
   a) Haja b) Bahati c) Umaskini d) Jitu e) Kuthamini
8. Kwa maoni yako ungechagua nini kati ya mali, akili na bahati? Kwa sababu gani? **(Alama 2)**

**SEHEMU YA II: MATUMIZI YA LUGHA NA SARUFI (Alama30)**

9. **Geuza katika wingi** **(Alama 10)**
   a) Chakula nikipendacho ni chapati kwa mboga ya mchicha.
   b) Jiko la stima atumialo mama ni jipya, limenunuliwa hivi majuzi.
   c) Rangi aipakayo mlangoni ni ya mafuta si ya maji.
   d) Mahali aishipo kuna majambazi na walevi wengi.
   e) Kalamu aitumiayo ni ya wino mwekundu ama wino mweusi?
10. **Andika kwa maneno** **(Alama 2)**
    a) 3,101,001 b)10,002
11. **Tia viambishi mwafaka katika nafasi zilizoachwa katika kila mojawapo ya maneno yafuatayo:** **(Alama 5)**
    **Mfano: Gari -angu -eusi-lianguka chini**
    **Gari langu jeusi lilianguka chini**
    a) Mtoto -le -dogo -likuwa -gonjwa.
    b) Meza hi- -pya -litengenezwa juzi na selemala -le.
    c) Kitabu -le -eupe ni -a baba -angu.
    d) Mto hu- -pana -refu -lifurika juzi -sivukike bila kutumia mtumbwi.
    e) Kifaru -le ndi- -li-nishambulia kishaye -katorokea katika msitu-le.

12. **Kamilisha vifungu vya maneno katika orodha A na vile katika orodha B ili kupata sentensi sahihi na yenye maana.** **(Alama 5)**

| ***A*** | ***B*** |
|---|---|
| a) Ngozi za wanyama | atabweka. |
| b) Farasi ana mbio | nzuri na tamu. |
| c) Panya ni wanyama | hutengenezwa viatu na mikoba. |
| d) Mbwa akimwona mwizi | kuliko ng'ombe na mbuzi. |
| e) Mbuzi wana nyama | waharibifu. |

13. **Jaza pengo kwa neno lifaalo miongoni mwa haya:** **(Alama 4)**
**Mionzi, kupendeza, kumetameta, darubini**
 a) Aliposherehekea siku yake ya kuzaliwa alivaa nguo za...
 b) Tunatumia ... kuangalia kitu kilicho mbali.
 c) ... kwa maua ni burudisho kwa macho ya watu.
 d) ... ya jua ndiyo inayotengeneza chakula cha miti.

14. **Andika maana mbili kwa kila sentensi.** **(Alama 4)**
 a) Amevaa miwani  b) Amechukua picha yangu

## SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 25)

15. **Jaza methali zifuatazo kisha ueleze kila moja kwa kifupi.** **(Alama 6)**
 a) Moja shika si ...  b) Mtegemea cha nduguye ...

16. **Eleza maana ya kila mojawapo ya nahau zenye mwandiko mzito katika sentensi zifuatazo:** **(Alama 3)**
 a) Maktabani kuna vitabu **chungu nzima.**
 b) **Hawakunipa mkono** nilipofaulu.
 c) Yule mama **alijifungua** mapacha mara mbili mfululizo.

17. Wahusika Bapa ni wahusika wa aina gani katika kazi ya fasihi? **(Alama 2)**

18. Katika shairi ulilolisoma hapo mwanzoni mwa nakala hii:
 a) Ni shairi la aina gani kulingana na idadi ya mishororo katika kila ubeti? **(Alama 2)**
 b) Mshororo wa mwisho katika kila ubeti unaitwa nini? **(Alama 2)**
 c) Toa mfano wa ukwapi na utao katika shairi hilo. **(Alama 4)**
 d) Eleza maana ya vina vya kati na vina vya mwisho ukitoa mfano kutoka shairi ulilolisoma hapo mwanzoni **Mali Akili Bahati.** **(Alama 6)**

## SEHEMU YA IV: UTUNGAJI (Alama 15)

19. **Chagua mada moja kati ya hizi mbili:**
 a) Tunga insha kuhusu " Umoja na Maridhiano kama njia ya maendeleo kwa Wanyarwanda baada ya mauaji ya kimbari".Usiandike chini ya maneno 200 wala juu ya maneno 210.
 b) Ulisoma katika gazeti moja tangazo likisema kuna ajira ya ukatibu katika wilaya ya Makolo. Muandikie barua meya wa wilaya hiyo ukiomba kazi hiyo ya ukatibu. Jina lako liwe Bahati.